# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS TAMISEMI

**MTIHANI WA UTAMILIFU KWA DARASA LA TATU 2020 (PESNO)**

**SIMU: 0713- 526533**

**0767- 526533**

## SOMO: KISWAHILI [04]

**TAREHE: 1 DECEMA 2020** **MUDA SAA: 1:30**

**JINA LA MTAHINIWA:** ____________________________________________________

**JINA LA SHULE**: __________________________________________________________

**WILAYA:** ________________ **MKOA:** ___________________

## MAELEKEZO:

1. **Jaza nafasi wazi hapo juu.**
2. **Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.**
3. **Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi.**
4. **Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa**

## IMLA

**1. Sikiliza kwa makini sentensi unazosomewa kisha uziandike kwa usahihi**

i. ____________________________________________

ii. ____________________________________________

iii. ____________________________________________

iv. ____________________________________________

v. ____________________________________________

**2. SARUFI NA MSAMIATI**

i. Neno, **“BARABARA”** lina idadi ngapi ya silabi

a. Mbili b. nne c. nane d. tatu [ ]

ii. Mtoto ______________ ambaye ataiba atapelekwa polisi

a. Yoyote b. yeyote c. wowote d. chochote [ ]

iii. Babu yangu hana meno kabisa mdomoni. Hivyo watu wengi humcheka na kumuita _________________

a. Toinyo b. chongo c. kiwete d. kibogoyo [ ]

iv. ____________ni siku inayofuata baada ya leo

a. kesho b. jana c. juzi d. kesho kutwa [ ]

v. Sisi sote _____________ kumsaidia babu kulima shamba kesho kutwa

a. tulikwenda
b. tumekwenda
c. tunakwenda
d. tutakwenda

[ ]

**3. FASIHI( METHALI, NAHAU NA VITENDAWILI)**

i. Tegua kitendawili kisemacho bibi yangu hachoki kunibeba

______________________________________________________

ii. Ni kitendawili gani ambacho jibu lake ni NANASI?

______________________________________________________

iii. Kamilisha methali ifuatayo

________________________________hujaza kibaba.

iv. Nahau anamkono wa birika ina maana gani?

______________________________________________________

v. Kamilisha methali hii. **Asiyesikia la mkuu**

________________________________________________

**4. UTUNGAJI**

**Tumia maneno yafuatayo kujaza nafasi zilizoachwa wazi**

| |
|---|
| kusuluhisha, busara, makubaliano, fujo, korongo, kuelewa |

Joshua alikuwa anakwenda sokoni. Alipofika njiani alikutana na kijana mmoja na kijana yule alianza kumletea (i) ______________________na kutaka kumsukuma ndani ya (ii) ______________________. Mara akatokea mzee mmoja mwenye (iii)_______________________ na kuamua (iv)________________________ mgogoro ule. Hatimaye aliwasihi vijana wale kufikia(v)_____________________

## 5. UFAHAMU

**Soma kifungu kifuatacho cha habari kisha ujibu maswali yanayofuata**

Siku moja Leah aliamka akiwa na homa kali. Mama yake alimpeleka zahanati ili kupata matibabu. Basi tabibu alimlaza yule binti na kumtibu kwa muda wa siku mbili. Leah alipata ahueni na kuruhusiwa kurudi nyumbani.

Alipofika nyumbani aliendelea na shughuli zake na hatimaye siku ya pili aliweza kuhudhuria masomo shuleni. Rafiki zake pamoja na walimu walifurahi kumuona tena lea na walikuwa naye bega kwa bega.

**MASWALI**

i. Ni nani aliyempatia Leah matibabu mara baada ya kufika zahanati?

____________________________________________

ii. Nini maana ya kupata ahueni?

____________________________________________

iii. Je, Leah alipelekwa hospitali na nani?

____________________________________________

iv. Nini maana ya nahau bega kwa bega?

____________________________________________

v. Leah alihudhuria masomo siku ya ngapi baada ya kutoka hospitali?

____________________________________________